TANESCO Makao Makuu, S.L.P. 453, Dodoma,Tanzania, Simu 180

# TAARIFA KWA UMMA

## CHANGAMOTO YA MANUNUZI YA UMEME KWENYE MFUMO WA LUKU

**APRILI 5, 2025.**

Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) linawataarifu wateja wake kuwa kuna changamoto kwenye manunuzi ya umeme (LUKU) inayosababisha wateja kushindwa kununua umeme kupitia mitandao ya simu na njia za kibenki kuanzia leo majira ya saa kumi na mbili na nusu asubuhi.

Wataalamu wetu wanaendelea na jitihada za kurekebisha changamoto iliyojitokeza ili kuwezesha manunuzi ya umeme kurejea kwenye hali yake ya kawaida.

Kwa sasa tunawashauri wateja kufanya manunuzi ya tokeni za umeme kupitia njia mbadala za mawakala waliopo nchi nzima wakati hatua za utatuzi zikiendelea.

Tutawataarifu huduma itakaporejea Shirika linaomba radhi kwa usumbufu wowote unaojitokeza.

**IMETOLEWA NA;**
**KURUGENZI YA MAWASILIANO NA HUDUMA KWA WATEJA,**
**TANESCO- MAKAO MAKUU,**
**DODOMA.**